SwahiliWeb

ELECTRONIC DEPOSITORY AND RESOURCE ARCHIVE

www.swahiliweb.net

Archive: Pat Caplan

Document: Mikidadi's diary

File reference: SW/PC/13033

This document has been downloaded from the SwahiliWeb archive on the understanding that it is copyright under the laws of the United Kingdom and the Berne Convention, and that no further copying, storage or distribution, in any form or by any means, including electronically, is permitted except under the provisions of fair dealing.

Copyright of all materials deposited with SwahiliWeb remains with the copyright holder. Those seeking copyright and associated permissions will be referred to the copyright holder.

**Extracts from Mikidadi Juma's tape-recorded diary, summer 2002, Kanga village**
**Transcribed by Joseph Bwathondi**

*Mikidadi, then aged 12, had kept a diary for me in 1966 when I had to leave the village for a month. In 2002, he was in his late forties, and had returned to Kanga to assist in my research. I asked if he would like to keep another diary, and he recorded it each evening for just over a week into my voice recorder. I have here omitted some very confidential material.*

***Part 1, tape 4. 22nd June-26th July 2002***

***22/6/2002 jumamosi***
Matukio muhimu. amafariki binti Pongwa yaani Rukia Pongwa na Jumapili amezikwa.
Prof amefika Kanga siku hiyo hiyo ya jumamosi.

***Tarehe 25/6/2002***
Bwana Mikidadi Manzi alisoma Hitima ya kuwarehemu wazee wake.

**Baraza la Kijiji**

Swali la pili itakuwaje kwa watakaokuwa hawakufika?
Jibu: utaratibu utafafanua juu ya suala hilo

Ajenda ya pili ilikuwa sekondari
Mwenyekiti aliwajulisha wananchi wajibu waliopanga wa kila mtu wa miji inayozunguka sekondari anayotaka kujengwa pale Kirongwe na Mvura kuenda kujitolea kwa siku atakayopangiwa mtu bila kukosa kuepuka usumbufu. Akaelezea pia kesho tarehe 22/7/2002 itakuwa siku ya wenyeviti wa vitongoji vyote vya Tarafa ya Kaskazini, na viongozi wote kwenda kuzindua ujenzi wa msingi wa shule hiyo.

Maswali: Hatibu Shomari Waziri alimuuliza mwenyekiti vipi kuhusu usafiri?
Jibu: kila mtu ajitegemee
Swali la pili : Je nikikosa kwenda kwa ugonjwa.
Jibu: viongozi wako watatoa maelezo yako huko Kirongwe kwa Wanaohusika ili wakutetee.
Swali la tatu : hivi kweli mtu anaweza kuondoka Kanga saa kumi ya usiku akaweza kujitolea pale Kirongwe?. Je mmeshindwa kututayarishia usafiri?
Jibu dogo: Labda tuchangie kidogo.
Muulizaji naye anasema: hatuwezi kumchangia mgeni atumie yaani katika kikao chapata joto la viongozi walifunga Ajenda.

Ajenda ya tatu: Ujenzi wa madarasa mawili Kanga.
Mwenyekiti aliita wito kwa kila kitongoji kitimize wajibu wake wa kujifyatulia matofalia mifuko 12 simenti kama ilivyopangwa ili kuharakisha ujenzi wa madarasa hayo.

Ajenda ya nne: Palizi ya mashamba ya minazi
Mwenyekiti akishirikiana na Katibu kata walieleza kuwa wasio palilia mashamba yao mpaka akija Hakimu mpya watashtakiwa mahakamani.
Maswali: Hatibu Shomari , je nyie viongozi mumo katika mpango huu au sisi raia tu?
b) Je vipi wenye mashamba yenye hati miliki wamo?
Mkutano wapata joto na ajenda zamalizwa mara moja.

 ©Pat Caplan 2013

Ajenda ya tano: Kodi ya maendeleo.
Katibu kata alipata nafasi badala ya mwenyekiti kueleza swala hili kwamba idadi kubwa ya watu hatujali kulipa kodi na muda wa kuongezeka kiasi kulipa faini umekaribia hivyo tujitahidi ili kila mmoja wetu alipe kodi mwaka huu mapema ili kuepuka usumbufu na kulipa zaidi pamoja na adhabu.

Ajenda ya sita Ugeni: Ajenda ya sita ambayo ilizungumzia ugeni yaani ujaji wa makamo wa raisi. Mwenyekiti wa wa kijiji mheshimiwa Muhsin Jabir aliwajulisha wananchi kuwa tunategemea kufikiwa na makamo wa raisi hapa kwetu Kanga na kufunguliwa/kufungua Zahanati yetu, hivyo tunawapa taarifa.

Maombi mzee Babu Jamali aliomba Afisa kilimo awe anakuja mara kwa mara kuhimiza kilimo chetu nakukiangalia.
Mohamed Salim Nassoro aliomba aitwe bwana Mipango ili aombwe kufatilia zao la nazi soko lake ili kuwainua wananchi na zao ili

Maswali: Hatibu Shomari aliuliza je haiwezekani kupata msaada wa kutoa maji machafu kisimani?
Jibu: Tujisaidie wenyewe ili tusaidiwe na hasa tujitegemee misaada haiwezekani.

Taarifa
Tujitahidi kujenga moyo wa kujitolea kwa mfano kijiji cha Bweni, wameazimia kujenga nyumba ya Mkunga nzuri zaidi kuliko ya Kanga. Wakaamua kuchimba msingi wa jingo hilo lote na wakaenda kwa Mkurugenzi wa kuomba msaada wa kujengewa, wakasubiri wakaamua kuchangishana shilingi 1000.00 kila mtu hadi hivi sasa hakuna aliyetoa na jengo limelala. Hapa wamekosa moyo wa kujitolea hivyo sisi tujitahidi kujenga moyo wa kujitolea kufanya mambo yetu wenyewe.

Haki Kwao yeye aliomba kumshukuru Prof Pat Caplan kwa moyo wake aliouonyesha kwa wananchi wa Kanga kwa kutengeneza kisima cha kitotoni.

Kabla ya mwisho mwenyekiti wa Serikali alimkaibisha kitogo Prof Pat Caplan aseme kidogo kwa wananchi naye alisimama na kusema “ nawashukuruni sana watu wa Kanga kwa kunipokea mara zote ninazokuja pamoja na mara hii ya tano . alisema yeye ni mwanafunzi wa watu wa Kanga na wao ni waalimu wake”.
Wananchi wote walifurahi kwa maneno hayo ya Prof Pat Caplan.

Kufungwa mkutano.
Mkutano ulimalizika saa kumi na moja na robo jioni kwa mwenyekiti kuwashukuru wananchi na kuwaelezea uzito walionao wananchi wanawake ambao alisema wajitahidi kubadilika ili twende na wakati na kwamba wao pia wanahitajika katika mikutano kwa na kwa hiyo ameomba tushirikiane juu ya swala hili. Mkutano uliudhuriwa na watu wapatao 50.

***22/7/2002***
**Mwaka mwaka mwaka kijiji Kanga**. Mwaka huu wa 2002. Mwaka Kongwa ulifanya tarehe 22/7/2002 sawa na mwezi 11 mwandamo 1423 hapa kijijini Kanga. Kuanzia majira ya saa moja mpaka saa Tano mchana katika vituo vya Rasini, Karibuni na Udongo. Watu wa rika tofauti wakiwemo wanawake , wanaume, wasichana na wavulana walikwenda Pwani kukoga mwaka kuagana na magonjwa na mabalaa ya mwaka uliopita. Na kukaribisha mwaka mpya. Mwaka huu watu wazima wa jinsia zote walikuwa kidogo mno hisipokuwa vijana wadogo wa kike na kiume wenye umri wa miaka 1 mpaka 15. Desturi ya zamani iliyokuwa ikifanywa siku ya mwaka


©Pat Caplan 2013

imeonekana mwaka huu kupungua yaani mikate kupelekwa Pwani kuliwa na watu wengi pamoja na nyimbo za asili na kutolewa Ada yaani mpunga mtama pesa kutoka kwa yule atakayetembelewa na watu wa Mwaka.

Mwaka huu nyimbo za asili na ada zimetolewa kituo cha Udongo tu. Karibuni pamoja na mikate kuliwa kwa wingi Pwani. Kama kawaida wakati wa jioni vijana wa kike na kiume walivalia nguo mpya na walifurika mitaani na Kichuni ambako kulipigwa ngoma ya kichengele ngoma ambayo si ya asili ya hapa Kanga. Ngoma ambayo asili yake ni ya kusini Mtwara na Lindi. Ngoma za asili za hapa Kanga ni kama vile **Kidatu Sonondo na Mkwaju** hazikuchezwa zaidi ya Kisengele. Vijana walishereheka na Video shoo na mipira ya miguu vijana wadogo. La kufurahisha ni kwamba wiki moja kabla ya siku ya mwaka mkubwa watu mbali mbali walisafisha makaburi lakini swala utoaji wa **Mafurungu** halikufanyika popote kijini Kanga. Aidha nimepiga picha matukio kadhaa ya mwaka.

***23/7/2002***
Nimepokea taarifa ya kifo cha mzee Bina kilichotokea Suta, Jimbo maziko yamefanyika leo hii.

Nimeendelea na kazi ya utafiti na mambo ya ukimwi, chakula pamoja na kushughulikia swala la kumpeleka Prof Caplan Bweni Panga ya **Tandawi na Kipena** kuona makaburi ya zamani.

Leo hii tumepata mvua za mwaka. Mvua hii imenyesha kidogo kidogo kuanzia majira ya saa moja na nusu usiku hadi saa mbili na nusu.

Tarehe hii hii 23/7/2002 niliweka matangazo ya sinema ambayo itaonyeshwa tarehe 25 na 26 sehemu za **Changwa, Mzambarahuni** na hotelini kwa Hamisi Yahaya Kanga . Na matangazo mawili niyapeleka kule Bweni. Kuwatangazia wananchi wa huko kuhusu suala hili.

Leo hii imeanika mpunga kwa ajili ya shughuli arubaini ya Rukia binti Pongwa itakoyofanyika mwishoni mwa wiki hii. Mpunga huo utatwangwa kesho tarehe 25/7/2002.
Kisengele imepigwa tena leo pale Kichuni kuendelea na sherehe ya mwaka Kongwa

**24/7/2002**
Nimeendelea na shughuli za utafiti wa masuala ya Ukimwi na kula chakula
Leo nimehoji watu wawili.

Nimepokea taarifa ya Umma kuachwa na mumewe, hivi sasa yupo nyumbani kwao Kurungeni kwa bibi yake Maalu.

Ujumbe unaokagua maeneo ya matunzaji ya mazingira umefika Kanga leo hii na kupitia baadhi ya maeneo kama vile shule ya msingi Bweni lakini hayakufika pale kwetu kwa Teacher.

**25/7/2002**
**Leo ni siku ya sinema** itayoonyeshwa na Prof Pat Caplan pale ofisini Kanga. Na sinema hii itaonyeshwa mfululizo leo na kesho. Sinema zitakazoonyeshwa ni Kilimo na mifugo huko UK na ile ya hapa Kanga iliyochukuliwa mwaka 1976 na watu wa BBC.

Vile vile leo ni siku ya **Utwanzi** wa mpunga kwa ajili ya arubaini na karamu ya Rukia binti Pongwa itakayofanyika Kirongwe mwisho/mwanzoni mwa mwezi ujayo

Tumepatwa na msiba wa watoto wetu Hassani Maji amefariki hospitali Kilindoni leo. Alipatwa na tatizo la Fansidar reaction
Leo jioni tutaonyesha sinema ambazo Pat Caplana amezileta.

***26/7/2002***
Sinema imefanyika na watu wengi wameudhuria, inafikiriwa kiasi cha watu wapatao 800 wameudhuria 350 wanawake na 400 wanaume walikuwepo na wageni toka Kilindoni kama vile Dr Naomi ,Hatibu, Mikidadi Mgeni, Mhamed Shea Driver na Amiri Dani mchezesha sinema. Sinema iliyokuwa ichezeshwe na Amiri Dani ilishindikana kwa sababu ya uzembe wake tu badala yake ikaonyeshwa video tu. Dr Naomi, Driver Mikidadi Mgeni na Amiri Dani waliondoka na gari usiku wa kama saa nne hivi kwenda Kilindoni.

Jenereta tuliyoitegemea kwa shughuli nzima ya kuonyeshea video kutoka Jojo pamoja na mawasiliano makubwa hakuja badala yake tulichuka ya hapa hapa Kanga pamoja na video screen. Prof Pat Caplan ambaye nilitegemea kufika Kanga mapema kwa ajili ya onyesho ili alifika saa moja na robo usiku akiwa mwenye uchovu na uzuni na hasiri na uchungu wakati hakujua kama onyesho litakuwepo kwa vile hata yeye alishaanza kuona dalili za kutofanikiwa onyesho hilo.

Tarehe hii ya 26/7/2002 ni siku ya maziko ya mtoto wetu Fatuma Hasan ambaye tunategemea kumzika saa nne asubuhi. Fatuma Hasan tumemzika leo asubuhi na tumemsomea **hitima.** Hitima inamalizika kesho asubuhi yaani saa mbili. Leo imekuwa hitma

Ehe leo imekuwa **hitimisho ya sinema** iliyotayarishwa na Prof Pat Caplan pale ofisini. Watu wengi wameudhuria onyesho hili la mwisho nadhani watu wapatao zaidi ya mia saba (700) wameudhuria wakiwemo watoto wadogo zaidi wa kiume na kike. Jambo ambalo halikuwapendeza wengi ni kuona kwamba watu wengi wamependelea sinema au video za vichekesho, ngoma, mpira nk lakini sio za mafunzo. Prof Pat mwaka huu ametuletea picha mbili mpya. Moja hakuonyeshwa na sababu ya Profjector na nyingine ya video imeonyesha ufugaji wa kondoo kule UK ambayo inaonyesha jinsi watu walivyo wanavyochunga kondoo wakitumia mbwa na farasi. Picha hii haikupendwa sana ikilinganisha na ile ya kanda iliyotayarishwa mwaka 1976 ambayo ni ya mambo yetu na hakuna jipya la kujifunza, ukiondoa mambo ya historia (mambo ya kale tu).

Kwa ujumla Prof Pat amefurahi mno kufanikisha onyesho ili. Siku ya kwanza honyesho lilifunguliwa na Mwenyekiti wa serikali ya kijiji kwa hotuba fupi ambayo aliitoa kumshukuru Prof Pat Caplan kwa kuonyesha sinema na kutoa misaada kijijini sehemu tatu, shule ya msingi Kanga iliyogharimu shillingi laki moja kwa ajili ya madawati, kukarabati kisima cha Kitotoni kwa gharama ya Tsh 84,000.00, kununua magodoro mawili, chandarua nne, mito mine mashuka manne yenye thamani ya Tsh 100,000.00 kwa ajili ya zahanati mpya ya Kanga.

Wananchi kwa upande wao wamefurahi sana juu ya misaada hiyo iliyotolewa na Prof Pat Caplan. Prof Pat Caplan naye alipata nafasi ya kujibu hotuba hiyo kwa maneno machache ya shukrani kwa watu wa Kanga kwa kumpokea vyema, kumkaribisha na kumfundisha mengi.

 ©Pat Caplan 2013

***28/7/2002***
Nimeendelea na shughuli ya utafiti siku nzima pamoja na kufatilia habari za makaburi ya zamani yaliyopo Ngome ambayo yamejengewa **vikuta** na baadhi ya vyombo vya nyumbani kama vile bakuli nk. Makaburi hayo yapo Ngome karibu na eneo lililozama meli mwaka 64 iliyojulikana kama Sukari Mawe. Kwa bahati nzuri Prof Pat aliwahi kutembelea sehemu hiyo kwa kupelekwa na marehemu Ali Abdalla Pori na amewahi Prof Pat kupiga picha makaburi hayo, lakini hayakutokea vizuri, uwezekano wa kuyafikia makaburi hayo tena imeshindikana baada ya kukosa mtu wa kutupeleka ambaye anapafahamu.

Watembeaji maharufu wa misituni yaani ngome kama vile Hatibu Juma Mchango, Juma Muhamed Kate, Vanya, Juma Athumani Mchie na Hatibu Manzi wote wameshindwa kupajua.

Leo pia kumefanyka **mafunzo rasmi chuoni yaani madrasa** kuhusu swala la kuhurumia wanyama na kuacha kuwaua hovyo. Mafundisho hayo yametolewa na Maalim Hamisi Omari mjumbe wa kamati ya madrasa kitengo cha mafunzo ambaye nilimuomba aje madrasa kuongea na wanafunzi juu ya suala hilo. Wanafunzi wote wameomba radhi juu ya jambo hilo na kuaidi kutorudia tena.

Jioni hii tumelikwa na Prof Pat Caplan kwenda kula chakula kwa maharusi Swalha na mumewe. Huko tulikuwa watu watano, bwana na bibi harusi, Prof Pat Caplan, Abdalla Musa Ali na mimi. Muda mfupi baada ya kuanza kula chakula Prof akapatwa na tatizo la kukwamwa na mwiba wa samaki wote tulishughulika na tulisimama kula mpaka nikatoa wazo la kumpatia Prof Caplan Chapati bahati nzuri mwiba ukaenda tumbani na tatizo hilo likawa limekwisha (***kicheko kwa mbali***) na tukaendelea na kula kama kawaida mpaka tukamaliza.Kwa kweli chakula kilikuwa kitamu na cha kutosha na maandalizi mazuri na kulipendeza sana. Na tuliondoka nyumba hiyo saa mbili na nusu usiku na tulifika nyumbani salama.

***29/7/2002***
Leo ni siku ya **kufunga mizigo na kuagana** na watu ambao Prof anahitaji kuagana nao. Ni siku ya kumalizia kutoa zawadi kwa watu mbalimbali aliozungumza nao na wale anaofahamiana nao. Watu aliozungumza nao aliwapa tochi kila mmoja hao ni Abdalla Ali, Seleman Ali, Ali Twaha Amiri, Hatibu Shomari Selemani Ali Yungi Mwanamvura Fatma Siku, Omari Mashi Mohamed, Muhsin Jabir, Maalim wa Madras, Selemani Bakari Afisa, alipewa kufuli mpya ya Shaba hisiyopungua thamani ya shillingi 2000.00.

Siku hii pia alitumia Prof Caplan kwa kulipa mishahara watu wote kama vile Fatma Shemsa,Teacher, mleta maziwa /muuza maziwa (Nassoro Hatibu). Prof Pat alimpatia Muhsin Jabir wenyekiti wa serikali ya kijiji kitabu cha Face Values kwa ajili ya kijiji cha Pangwa.

***30/7/2002***
Leo hii tumekuwa tukimalizia kufunga mizigo ya Prof Pat Caplan ambayo anachukua kwake London pamoja na zawadi alizotayarisha kwa marafiki zake wa Kilindoni, Mwembeni na Utende. Tumekuwa tunangojea gari ya kwenda Kilindoni ambako tutakuwa mpaka tumalize kazi tuliyonayo huko. Tumepata gari jioni saa nane na dakika 54 na tunaondoka kwenda Kilindoni na mizigo yetu, mimi na Prof Pat Prof Pat alikutana na wanafunzi wa Chuo /Madrasa nakuagana nao na kuwazungumzia maneno machache ya kuwaaga. Watoto waliuzunika na Prof alizunika pia. Prof alitokwa na machozi wakati alipokuwa akiaga Kanga na alipiga Kimya kizito kilichochukua kama dakika kumi.

Tulipofika Kilindoni tulipita hospitali kumuona mke wa mzee Salum Nassoro anayeugua hapo hospitalini pamoja na Fatma Salum ambaye pia aliyepatwa na homa ya malaria wakati akimuuguza mama yake. Pale hospitali tuliwakuta Fatma Salum, Hadija Salum, Salehe Salum, Selemani Salum Selemani, Maharufu na wanawake wawili wageni na hali ya mgonjwa haikuwa nzuri. Jioni tulifika. Harbor View Resort na tulikuta chumba kwa Pat Caplan kilikuwepo. Jioni ya saa kumi na moja na dakika 40 Prof alimkaribisha Dr Naomi na Mumewe Soda Pale Harbor view pamoja na mazungumzo mafupi hadi. Saa Moja na dakika 45 usiku na kuagana nao. Wakati wa kugana nao Prof Pat Caplan tuliondoka naye hadi sehemu inayouzwa chapati na samaki wa kukaanga ambapo alipata kununua chapatti na samaki kwa chakula chake cha jioni.

Prof Pat Caplan amenilipa sh 4200/= kwa ajili ya matengenezo ya matofali.

***31/7/2002***

Pia alifanya mawasiliano na Catherine Mtembei pale kwa muheshimiwa mbunge Tarehe 31/7/2002 tumekwenda kumjulia hali mke wa Salum Nasoro pale hospitali Kilindoni na tukakutana na mzee Salum Nasoro mwenyewe.Hali ya mgonjwa tumeikuta afadhali. Tumepokea taarifa ya kuja kwa waganga pale Kanga wakitokea Bweni kutafuta uchawi. Pale Kanga wamefika nyumbani kwa Hija Ngweshani taarifa tulizozipata zaidi zinasema baadhi ya watu hawataki watu hawa wachawi waje Kanga. Maana hawaamini sijuhi itakuaje hapo baadae. Mzee Salum Nasoro yeye amesema hawataki kuja kwake sawa na mimi.

Nimepokea shs 3000 hapa nimeacha nimepokea shs 10000.00 kabla ya tarehe 31/7 kwa ajili ya matumizi yangu. Nimepokea Tshs 3000.00 zingine za chakula changu.

Mchana huu tulipita sokoni kupata mahitaji na baadae kuelekea Harbor View. Tumeenda pia Mwembeni kumuona Jeansen na kumpa zawadi ya mkeka na Prof Pat Caplan pamoja na kumkaribisha kinywaji kesho jioni. Tulienda huko na gari ya hoteli kwa gharama nafuu ya mafuta ya lita tano. Tulirudi hotelini na kuendelea na kazi zetu.

 ©Pat Caplan 2013